
# Kusoma

## Kitabu cha Mwanafunzi

Darasa la Pili




Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kusoma

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Pili



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 5

Jina la Chapisho: Kusoma Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Pili

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978 - 9976 - 61 - 705 - 4

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 19 Mwezi Januari Mwaka 20 18 kuwa kitabu cha Kiada kwa ajili ya Darasa la Pili katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2015.

**Dkt. Edicome Cornel Shirima**
Kaimu Kamishna wa Elimu.

## Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

KUSOMA DARASA LA PILI.indd 1 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la kwanza 2018

ISBN 978 - 9976 - 61 - 705 - 4

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam

| | |
|---|---|
| Simu | +255 735 041170/ +255 735 041168 |
| Baruapepe | director.tie@tie.go.tz |
| Tovuti | www.tie.go.tz |

FOR ONLINE USE ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 2 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Utangulizi**.....................................................iv

**Shukurani**.......................................................v

**Sura ya Kwanza**
Kuzungumza.........................................................1

**Sura ya Pili**
Kutambua na kuunganisha sauti za herufi....................12

**Sura ya Tatu**
Kutambua sauti za herufi dh, th na ng'..................... 20

**Sura ya Nne**
Kutamka sauti zinazounda maneno.................................24

**Sura ya Tano**
Kutambua sauti za herufi ngw, nyw, mbw, chw na ndw....31

**Sura ya Sita**
Kusoma kwa ufahamu..................................................35

**Sura ya Saba**
Kusoma kwa ufasaha...................................................41

**Sura ya Nane**
Kusoma hadithi fupi....................................................47

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 3 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kujua kusoma ni muhimu katika kujifunza. Ukijua kusoma utaweza kujifunza mambo mengi. Utaweza pia kumudu masomo yako mengine unayofundishwa shuleni.

Kitabu hiki kitakuwezesha kujua kusoma vizuri. Kwa kusoma kitabu hiki utaweza kuzungumzia michezo, kusimulia matukio na hadithi. Aidha, utaweza kuunganisha sauti za herufi ili kuunda silabi. Kuunganisha silabi, kuunda maneno na kuunda sentensi. Utaweza pia kusoma kwa ufasaha na ufahamu.

Kitabu hiki kina maswali, mazoezi na mifano mbalimbali. Jibu maswali na fanya mazoezi yaliyomo kitabuni. Iwapo utashindwa kujibu maswali au mazoezi waulize wenzako. Unaweza pia kuwauliza wazazi, walezi au walimu wako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi na maandalizi ya kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui na uhariri wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa ukaribu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.



**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 5 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


# Sura ya Kwanza

## Kuzungumza

### Kuzungumzia michezo

**Tazama picha zifuatazo kisha jibu maswali.**

1



2



FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 1 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Unaona nini katika picha namba 1 na 2?
2. Michezo gani inachezwa katika picha namba 1 na 2?
3. Kwa nini wanafunzi wanapenda kucheza michezo hiyo?
4. Je, michezo ina faida gani?
5. Je, wewe unapenda mchezo upi kati ya hiyo?

**Soma mazungumzo haya kisha jibu maswali.**

**Baraka** Furaha, hujambo?
**Furaha** Sijambo.
**Baraka** Jana ulikwenda kuangalia mazoezi ya mpira?
**Furaha** Ndiyo.
**Baraka** Mimi sikuweza kwenda. Je, unaweza kunisimulia kidogo?
**Furaha** Ndiyo, kulikuwa na mazoezi ya mpira wa miguu.
**Baraka** Je, ni timu gani zilikuwa zinafanya mazoezi?
**Furaha** Kulikuwa na timu ya wasichana na wavulana.
**Baraka** Hee! Wasichana nao walicheza mpira wa miguu?
**Furaha** Ndiyo, tena walicheza vizuri sana.
**Baraka** Loo! Nimefurahi kusikia hayo.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 2 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



## Maswali

1. Nani alikwenda kuangalia mpira?
2. Uwanjani kulikuwa na timu zipi?
3. Timu gani ilicheza vizuri?
4. Kwa nini Baraka alifurahi?
5. Mazungumzo kati ya Furaha na Baraka yanatufundisha nini?



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 3 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

Igiza mazungumzo ya Baraka na Furaha.

**Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali.**

## Zakaria mkimbiaji

Zakaria anasoma darasa la pili. Yeye na rafiki zake walipenda mchezo wa kukimbia. Zakaria alipenda zaidi michezo kuliko masomo ya darasani. Wazazi wake hawakuipenda tabia hiyo.

Siku moja mjomba wake, aliongea na Zakaria. Alimweleza umuhimu wa kusoma kwa bidii. Vilevile, alimweleza faida za michezo. Zakaria aliamua kubadilika. Aliongeza juhudi katika masomo na michezo. Zakaria akawa mwanafunzi bora darasani. Alifanya vizuri mitihani ya kuingia darasa la tatu. Walimu na wazazi wake walifurahi sana.


Zakaria alishiriki mashindano mbalimbali ya michezo. Alifanya vizuri katika mashindano hayo. Zakaria alipata zawadi ya vitabu na vyeti.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 4 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Alipewa jina la Zakaria Mkimbiaji kwa uhodari wake. Wazazi na mjomba walifurahishwa na maendeleo ya Zakaria.

## Maswali

1. Zakaria na rafiki zake walikuwa wanapenda nini?
2. Nani alimweleza Zakaria umuhimu wa kusoma kwa bidii?
3. Kwa nini Zakaria alifanya vizuri katika masomo na michezo?
4. Zakaria alipata zawadi gani?
5. Habari hii inatufundisha nini?



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 5 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Kusimulia hadithi

**Maswali**

1. Je, uliwahi kusimuliwa hadithi?
2. Je, hadithi hiyo ilihusu nini?
3. Unaposimulia hadithi unaanzaje?
4. Wasimulie wanafunzi wenzako hadithi yoyote unayoifahamu.

**Soma hadithi ifuatayo kisha jibu maswali.**

### Kibakuli aacha uchafu



Kibakuli na Mariamu ni ndugu. Wote walisoma darasa la pili. Baba yao aliitwa Yusufu. Mama yao aliitwa Sara. Wote waliishi mtaa wa Mwembeni, jijini Maendeleo. Mariamu alikuwa anapenda kuwa msafi wakati wote. Alifua nguo za nyumbani na sare za shule.

Kila siku asubuhi alioga na kupiga mswaki. Alivaa sare safi ya shule.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 6 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kibakuli alikuwa mvivu sana. Hakupenda kuoga wala kupiga mswaki. Hakupenda kufua nguo za nyumbani wala za shule. Pia, hakupenda kuchana nywele zake. Mariamu alimwambia Kibakuli aache uchafu lakini hakusikia.

Baada ya mwezi mmoja Kibakuli alianza kujikuna. Wenzake walimweleza kuwa anajikuna kwa sababu ya uchafu. Walimweleza kuwa akiwa msafi hatajikuna tena.

Muda wa masomo ulipomalizika, Kibakuli aliondoka kuelekea nyumbani. Alipofika nyumbani, alibadili nguo zake. Alimwomba baba yake amkate nywele pamoja na kucha. Alichukua ndoo yenye maji na sabuni kisha akaoga. Baada ya kuoga, Kibakuli alivaa nguo safi. Alichana nywele zake, akapendeza sana. Kibakuli hakujikuna tena. Aliahidi kuwa msafi kila siku.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 7 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Kibakuli na Mariamu waliishi wapi?
2. Kibakuli alikuwa na tabia gani?
3. Je, tabia ya Kibakuli ilimletea matatizo gani?
4. Je, Kibakuli angekuwa ndugu yako ungemsaidiaje?
5. Msimulie rafiki yako hadithi uliyoisoma.

## Zoezi la 2

1. Soma na tamka sauti za mwanzo za maneno.

   safi kuoga zake vile

2. Soma na tamka sauti za mwisho za maneno.

   sare nguo siku mswaki tena

3. Eleza maana ya maneno kwa kuchagua jibu sahihi.

| Maneno | Maana |
|---|---|
| 1. Sare | mtu asiyependa kujituma. |
| 2. Mvivu | nguo zinazofanana. |
| | nguo za rangi ya kijani. |

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 8 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kusimulia matukio


### Maswali

1. Je, umewahi kwenda kwenye sherehe yoyote?
2. Ilikuwa sherehe ya nini?
3. Wasimulie wenzako kuhusu sherehe hiyo.

**Soma habari hii kisha jibu maswali.**

### Sherehe ya dada

Mimi ninaitwa Amani. Dada yangu anaitwa Sada. Mdogo wangu anaitwa Heri. Tunaishi na wazazi wetu katika Kijiji cha Magunga. Kijiji chetu kiko mkoa wa Tanga. Mwaka uliopita dada yangu alimaliza mafunzo ya udaktari. Alisoma katika Chuo Kikuu cha Muhimbili.



FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 9 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Dada aliporudi nyumbani wazazi waliandaa sherehe ya kumpongeza. Waliwaalika ndugu, majirani na marafiki. Siku hiyo dada alivaa vazi zuri sana.Vazi hilo linaitwa joho. Joho ni vazi refu, pana lililo wazi mbele. Hudariziwa kwa nakshi mbalimbali. Vilevile, alivaa kofia. Dada alipendeza sana. Alikaa kwenye kochi lililopambwa kwa vitambaa vizuri. Mimi na mdogo wangu tulikaa karibu na dada.

Wageni walipofika walipewa chakula na vinywaji mbalimbali. Wote walifurahi sana. Baada ya kumaliza kula walimpa dada zawadi. Alipata zawadi ya fedha na vitu mbalimbali. Baadaye watu wote walicheza ngoma hadi sherehe ilipokwisha.

Heri alimuuliza dada, kwa nini wazazi wamekufanyia sherehe? Mimi pia nataka wanifanyie sherehe kama hii. Dada alimjibu, kwa sababu nimemaliza mafunzo ya udaktari. Nimefaulu vizuri mitihani yangu. Heri alimuuliza tena, ulifanyaje hadi ukafaulu mitihani yako? Dada alijibu, nilisoma kwa bidii sana. Heri akasema, mimi pia nitasoma kwa bidii.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 10 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Dada yake Amani alisoma chuo gani?
2. Kwa nini Sada alipongezwa na wazazi wake?
3. Heri alimuuliza nini dada yake?
4. Kwa nini Heri alisema kuwa atasoma kwa bidii?
5. Msimulie mwenzako hadithi hii.

## Zoezi la 3

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi.**

joho jirani kumualika kumpongeza daktari

1. Mtu anayetibu wagonjwa huitwa.......................
2. Kumpa mtu hongera kwa jambo zuri alilofanya

   ..........................................................................
3. Kumkaribisha mtu nyumbani ni .........................
4. Vazi refu pana lililo wazi mbele huitwa ..............
5. Mtu anayeishi karibu na mtu mwingine ni...........

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 11 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Kutambua na kuunganisha sauti za herufi

### Kuhusianisha sauti na herufi

bB, mM, kK, dD, nN, lL, tT, pP, sS,fF,

jJ, gG, yY, zZ, hH, rR, wW, vV.

**Soma habari hii kisha jibu maswali.**

### Azimio na Maua

Siku moja Azimio alimwambia Maua, muangalie **huyu** mwanafunzi. Anaweza kutamka sauti za herufi. Je, **wewe** unaweza? Kama huwezi nitakufundisha.

Azimio aliendelea kusema, mwalimu wetu alitufundisha vizuri. Alituambia tunaweza kutamka sauti za herufi kwa **urahisi**. Tunatakiwa kutamka maneno **mengi** yenye sauti tunayojifunza. Neno **f**agia sauti ya mwanzo ni **f**.

Kisha, Azimio alitamka maneno **s**aa, **s**asa na **s**ita. Sauti ya mwanzo ya maneno hayo ni ipi? Maua alijibu kuwa sauti ya mwanzo ni **s**. Azimio alifurahi sana na kumwambia Maua sasa umeelewa.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 12 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

**Jibu maswali haya.**

1. Soma kwa sauti maneno yaliyokolezwa wino katika habari.
2. Tamka sauti za mwanzo za maneno hayo.

**Mfano** Neno **s**ita sauti ya mwanzo ni s.

3. Tafuta maneno yenye sauti zifuatazo katika habari uliyosoma.

n t h y z k m

4. Soma maneno hayo kwa sauti.
5. Tamka sauti za herufi hizi

b, M, k, D, n, L, t, P, s, F, j, G, Y,

z, H, r, W, v, Ch, B, m, K, d, N, l, T,

p, S, f, J, g, y, Z, h, R, w, V, ch

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 13 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuunganisha sauti za herufi ili kuunda silabi

Unganisha sauti za herufi p ch g v y z j m h w na o u i a e ili kuunda silabi.

**Mfano**

Ukiunganisha sauti ya herufi p na sauti ya herufi i Unaunda silabi pi

p i pi

Tazama mifano mingine

g e ge

h a ha

### Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Unganisha sauti za herufi t ch g v p h z d j w na o e i a u ili kuunda silabi kumi.
2. Tenganisha na tamka sauti za herufi zinazounda silabi.

| | | |
|---|---|---|
| **Mfano** ge | g | e |
| chu | ____ | ____ |
| po | ____ | ____ |

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 14 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuunganisha silabi ili kuunda maneno

**Imba wimbo huu.**

### Wimbo wa Silabi

Silabi ya mwanzo katika neno ua ni u
Tusome sote kwa pamoja silabi u, u, u.

Silabi ya mwanzo katika neno oa ni o
Tusome sote kwa pamoja silabi o, o, o.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali haya.**

1. Unganisha silabi a, e, i, o na u kuunda maneno.

**Mfano** Ukiunganisha silabi o na a unaunda neno oa

| | | |
|---|---|---|
| o | a | oa |
| u | ____ | ____ |
| a | ____ | ____ |

2. Soma maneno uliyounda kwa sauti.

3. Tenganisha silabi zinazounda maneno haya.

| | | |
|---|---|---|
| ua | ____ | ____ |
| oa | ____ | ____ |

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 15 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuunganisha silabi ili kuunda maneno yenye silabi tatu

Soma kwa sauti silabi zilizomo katika chati. Fanya zoezi linalofuata.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| de | ha | pe | ti | u | the | a | m | cha |
| ku | ta | **li** | mu | wi | lu | di | no | **za** |
| **su** | **lo** | wi | fi | ki | hi | bi | me | la |
| ka | ha | mi | **ma** | na | ga | ye | **ri** | ye |
| wo | **ni** | pa | bu | ya | zu | de | zi | we |
| sa | ba | che | ke | **ka** | ru | zo | mu | tu |
| ku | re | **go** | ki | he | si | pi | u | ga |

### Zoezi la 3

Unda maneno yenye silabi tatu kwa kutumia chati.

**Mfano** sukari zamani gololi

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 16 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

**Jibu maswali haya.**

1. Kamilisha maneno kwa kutumia silabi hizi.

**li cho ki wa m**

da __ ti
mka__
tu ____ re
__zazi
fi ____ a

2. Tenganisha na tamka silabi zilizounda maneno haya.

mayai nunua somewa fikiri mlima

3. Soma maneno haya yasiyo na maana kwa sauti.

| | | | |
|---|---|---|---|
| pamka | kirafi | tekami | mulimwa |
| risuka | aruki | tomto | nduweku |
| varede | nimbasha | nimitha | ngunamwa |
| rapim | | | |

4. Panga maneno haya katika silabi ili yalete maana.

**Mfano** tomto mtoto

| | | | |
|---|---|---|---|
| pamka | kirafi | tekami | mulimwa |
| risuka | aruki | tomto | nduweku |
| varede | nimbasha | nimitha | ngunamwa |
| rapim | | | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

### Kuunganisha maneno ili kuunda sentensi

1. Soma maneno haya kwa sauti.

   Daktari   Mwanafunzi   Mvuvi   Dereva   Mfugaji

2. Panga maneno yafuatayo ili kuunda sentensi sahihi.



**Mfano**

mgonjwa Daktari anampima.

Daktari anampima mgonjwa.



anaendesha Dereva gari.

..................................




samaki anavua Mvuvi.

..................................

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mfugaji maziwa anakamua.



.........................................

kitabu Mwanafunzi anasoma.



............................................

## Zoezi la 6

### Kutenganisha maneno yaliyounda sentensi

Tenganisha maneno yaliyounda sentensi.

**Mfano** Mwalimuanafundishavizuri.

Mwalimu anafundisha vizuri.

1. Kakaanachezampira.
2. Tusiokotevituovyo.
3. Mtotomdogoanalia.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 19 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


# Sura ya Tatu

## Kutambua sauti za herufi dh, th na ng’

**Soma habari hii kisha fanya zoezi linalofuata.**

### Mzee Mkali

Juma anaishi na wazazi wake katika Kijiji cha Mtakuja. Baba yake anaitwa Mkali. Mzee Mkali ni mfanyabiashara. Siku moja Mzee Mkali alikwenda sokoni kuuza **bidhaa.**



Alipofika, alimkuta mlinzi amesimama mbele ya soko. Mlinzi akamuuliza, kwa nini umewahi sana? Mzee Mkali akajibu, nataka nianze kuuza bidhaa mapema.



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 20 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mlinzi akamuuliza tena, bidhaa zako zina **thamani** gani? Mzee Mkali akajibu, naona unanitania. Thamani yake ni kubwa siwezi kukuambia. Mlinzi akasema, nisamehe bwana. Mlinzi alichukua rangi ya viatu na kuanza **kuving'arisha**. Hakuendelea tena kuongea na Mzee Mkali.

## Zoezi la 1

1. Soma kwa sauti maneno yaliyokolezwa wino.
2. Unganisha sauti za herufi **dh th ng'** na **o e i a u** kuunda silabi.

**Mfano**

| | | |
|---|---|---|
| dh | a | dha |
| th | ___ | ___ |
| ng' | ___ | ___ |

## Zoezi la 2

1. Soma kwa sauti silabi hizi.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| dha | thu | ng'i | DHU | ng'o | dhe |
| dhi | THA | ng'e | dho | thi | dhu |
| DHA | tho | ng'a | NG'O | tha | ng'u |

2. Tenganisha sauti za herufi zinazounda silabi hizi.
   **dha** **ng'o** **tha**

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 21 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

**Jibu maswali haya.**

1. Kamilisha maneno yafuatayo kwa kutumia silabi hizi.

ng'a thi ra dha dhi the

**Mfano**

| | |
|---|---|
| ___habu | dhahabu |
| mara___ | ______________________ |
| thelu ___ | ______________________ |
| __lathini | ______________________ |
| ___rau | ______________________ |
| ___risha | ______________________ |

2. Tenganisha silabi katika maneno kwa kuzisoma kwa sauti.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mfano** | ng'arisha | ng'a | ri | sha |
| | dhaifu | ___ | ___ | ___ |
| | theluthi | ___ | ___ | ___ |
| | mng'ao | ___ | ___ | ___ |

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 22 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

**Jibu maswali haya.**

1. Chagua maana ya kila neno katika jedwali lifuatalo.

| Maneno | Maana |
|---|---|
| 1. Bidhaa<br>2. Thamani<br>3. Ng'arisha | ubora wa kitu au gharama yake. |
| | vitu vinavyoweza kuuzwa au kununuliwa. |
| | fanya kitu kimeremete ili kipendeze. |
| | vaa viatu. |

2. Tunga sentensi sahihi kwa kutumia jedwali hili.

**Mfano** Kaka amenunua bidhaa nyingi.

| | | |
|---|---|---|
| Kijana huyu<br>Baba<br>Kaka | amenunua<br>ameng'arisha | bidhaa nyingi.<br>viatu vyake.<br>vifaa vya thamani. |

3. Tenganisha maneno yaliyounda sentensi zinazofuata baada ya mfano.

**Mfano** Mamaamenunuabidhaambalimbali.
Mama amenunua bidhaa mbalimbali.

Dadaameng'arishaviatuvyake.
Babaamepatafedhanyingi.
Shangaziamenipashilingithemanini.
Kakaamepatadhahabu.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 23 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Kutamka sauti zinazounda maneno

**Soma habari hii kisha fanya zoezi.**

### Mwalimu wetu

Mimi ninaitwa Kulwa. Mdogo wangu anaitwa Doto. Doto ni pacha wangu. **Sote** tunasoma **darasa** la pili. Mwaka **jana** tulikuwa darasa la kwanza. Mwalimu wetu anaitwa Masawe. Anatufundisha **kusoma**, kuandika na kuhesabu. Mwalimu wetu anatufundisha vizuri.






KUSOMA DARASA LA PILI.indd 24 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sisi sote tunajua kusoma, kuandika na kuhesabu. Mimi ninaweza kusoma maneno kama simu na chupa. Pia naweza kusoma maneno meza na shati. Tulipokuwa darasa la kwanza, tulijifunza sauti za **herufi**. Mwalimu alitufundisha kutambua **sauti** hizo kwa kuimba nyimbo. Tulifanya pia mazoezi ya kutambua sauti za herufi. Mwalimu alituambia tutaendelea kujifunza sauti zinazounda maneno mbalimbali.


## Zoezi la 1

1. Soma kwa sauti maneno yaliyokolezwa wino katika habari.
2. Tamka sauti zinazounda maneno haya.

sauti jana sote darasa kusoma herufi

**Tazama picha hizi kisha fanya zoezi linalofuata.**

1


2


3


4


FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 25 24/07/2021 13:11


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2


**Jibu maswali haya.**


1. Taja majina ya picha namba 1 hadi 4.
2. Tamka sauti zinazounda majina ya vitu hivyo.
3. Mwambie rafiki yako atamke neno lolote, **mfano** kula.
4. Tamka sauti zinazounda neno hilo.


**Tazama picha hizi kisha fanya zoezi.**

1


2


3



4


5


FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 26 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

**Jibu maswali haya.**

1. Taja majina ya picha namba 1 hadi 5.
2. Neno dawati lina silabi ngapi?
3. Tamka silabi zinazounda majina ya vitu katika picha.

   **Mfano** fa gi o
4. Tamka sauti za mwanzo zinazounda majina hayo.
5. Tamka sauti za mwisho zinazounda majina hayo.

## Zoezi la 4

**Jibu maswali haya.**

1. Tamka sauti za neno unalolijua lenye silabi tatu.

   **Mfano** k u s o m a
2. Mwambie rafiki yako aunganishe sauti hizo kuunda neno.
3. Mwambie rafiki yako atamke sauti za neno

   **Mfano** d a w a t i
4. Unganisha sauti hizo ili kuunda neno.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 27 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Zoezi la 5

Taja idadi ya sauti za herufi zinazounda maneno katika jedwali.


| Neno | Idadi ya sauti |
|---|---|
| chakula | sita |
| mdogo | |
| kulia | |
| dodoki | |
| mchicha | |

**Tazama picha hizi kisha fanya zoezi.**

1



2



FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 28 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 6

**Jibu maswali haya.**

1. Taja majina ya picha namba 1 na 2.
2. Tamka sauti za herufi za mwisho zinazounda majina hayo.
3. Badili sauti ya mwisho ya neno bati. Weka sauti a. Je, umepata neno gani?
4. (a) Tamka sauti za mwisho za maneno haya.
   chota yako koti mwaka wapi
   (b) Badili sauti ya mwisho kuwa **e** katika maneno.
   Je, umepata maneno gani?

## Zoezi la 7

Badili sauti za mwisho katika maneno haya. Tumia sauti za herufi e o u i a kuunda maneno mapya.

**Mfano**

Sauti ya herufi ya mwisho ya neno pipa ni a. Ukiweka sauti i mwishoni unapata neno pipi.

| | |
|---|---|
| pipa | pipi |
| chake | _ |
| vita | _ |
| kata | _ |
| kita | _ |
| lake | _ |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 8

Badili sauti za mwanzo katika maneno. Tumia sauti za herufi b s p n k t kuunda maneno mapya.

**Mfano**

Sauti ya mwanzo ya neno taa ni **t**. Ukiweka sauti ya herufi **s** mwanzoni unapata neno **s**aa.

taa saa

pata _

kaa _

pita _

toa _

bua _

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 30 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Kutambua sauti za herufi ngw, nyw, mbw, chw na ndw

### Kuhusianisha sauti na herufi

**Soma habari hii kisha jibu maswali.**

### Faraja

Faraja anaishi na wazazi wake. Baba yake anaitwa Juma. Mama yake anaitwa Pendo. Juma na Pendo ni wafanyabiashara. Wazazi hao wana duka kubwa lenye bidhaa mbalimbali. Faraja akitoka shuleni huwasaidia kazi wazazi wake. Huwasaidia kuuza bidhaa za dukani.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Faraja alimwambia baba yake kuhusu somo walilojifunza shuleni. Alimwambia, walijifunza jinsi ya kukusanya na kuhesabu vitu. Wamejifunza pia kupanga vitu katika makundi yanayofanana.

Faraja alitaka kutumia ujuzi wake wa kupanga vitu. Alimwomba baba yake wapange wote bidhaa za dukani. Baba yake alifurahi sana. Alimweleza Faraja kuwa, bidhaa zinapaswa **kupangwa** vizuri. Kupanga bidhaa vizuri huvutia wanunuzi. Aidha, bidhaa zinatakiwa kuhesabiwa ili kujua idadi yake.

Hatimaye, Faraja na baba yake walianza kupanga bidhaa. Faraja **aliombwa** apange bidhaa sehemu anayoweza kufikia. Watu waliopita karibu na duka hilo walimshangaa Faraja. Waliona jinsi alivyokuwa anapanga bidhaa vizuri. Faraja na baba yake walimaliza kazi mapema. Kazi **iliyofanywa** na Faraja ilimfurahisha sana baba yake. Aliahidi kumnunulia Faraja zawadi. Faraja **anapendwa** sana na wazazi wake.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Faraja anaishi na nani?
2. Baba yake Faraja anafanya kazi gani?
3. Faraja alijifunza nini shuleni kwao?
4. Kwa nini Faraja alitaka kupanga bidhaa za dukani?
5. Kwa nini watu walimshangaa Faraja?
6. Habari hii inatufundisha nini?



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 32 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Soma kwa sauti maneno yaliyokolezwa wino katika habari.
2. Tamka silabi za mwisho zinazounda maneno hayo.
3. Neno **aliombwa** lina silabi ngapi?

## Zoezi la 2

1. Unganisha sauti za herufi mbw ngw chw nyw ndw na o i u a e kuunda silabi.

   **Mfano**

   Sauti za herufi mbw na e unapata silabi mbwe.

   | | |
   |---|---|
   | mbw e | mbwe |
   | ngw a | ngwa |
   | chw a | _____ |
   | nyw e | _____ |
   | ndw a | _____ |

2. Soma silabi zifuatazo kwa sauti.

   mbwe NGWA ndwe CHWI nywe
   NDWE ngwa MBWE chwi NYWE

3. Tenganisha sauti za herufi zinazounda silabi hizi.

   **Mfano**

   | | | |
   |---|---|---|
   | chwi | chw | i |
   | ndwa | ____ | __ |
   | mbwe | ____ | __ |



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 33 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

1. Soma maneno haya kwa sauti.

nywele ngwara mbweha pendwa mchwa

2. Tenganisha silabi zinazounda maneno haya.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mfano** | nywele | nywe | le |
| | mchwa | ____ | ____ |
| | mbweha | ____ | ____ |
| | pendwa | ____ | ____ |

3. Soma maneno haya yasiyo na maana.

| | | |
|---|---|---|
| hambwe | ndwape | chwaki |
| rangwa | pwam | lenywe |

4. Panga maneno hayo katika silabi mbili yalete maana. **Mfano** hambwe mbweha

## Zoezi la 4

1. Tunga sentensi sahihi kwa kutumia jedwali hili.

**Mfano** Mbweha ni mnyama wa porini.

| | | |
|---|---|---|
| Mbweha<br>Chungwa hili<br>Nywele zake<br>Mchwa | ni | tamu sana.<br>fupi sana.<br>mnyama wa porini.<br>sehemu ya mwili.<br>ndefu.<br>mdudu. |

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 34 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Kusoma kwa ufahamu


### Kutabiri matukio

**Jibu maswali haya.**

1. Mvua ikinyesha kupita kiasi kutatokea nini?
2. Usipopiga mswaki kutatokea nini?
3. Upepo mkali ukivuma kutatokea nini?

**Tazama picha zifuatazo kisha tabiri kinachoweza kutokea.**

1







KUSOMA DARASA LA PILI.indd 35 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2



3





KUSOMA DARASA LA PILI.indd 36 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


**Soma hadithi ifuatayo kisha jibu maswali.**

## Bibi Chausiku

Hapo zamani za kale, alikuwepo bibi mmoja. Jina lake aliitwa bibi Chausiku. Alipenda kufanya kazi kwa bidii. Siku moja aliamka mapema kwenda porini kutafuta kuni. Alipofika porini, alikusanya kuni na kuzifunga kwa kamba. Wakati akitembea porini, alichomwa na mwiba mguuni. Akakaa chini kwa huzuni.

Mara alipita kijana mmoja. Kijana huyo aliitwa Jumanne. Jumanne alimsalimia bibi. Bibi aliitikia salamu na kumwomba amtoe mwiba. Bibi alisema, mjukuu wangu, naomba unitoe mwiba. Jumanne alimsogelea bibi na kumtoa mwiba. Bibi alimshukuru sana. Alimwambia, asante sana mjukuu wangu.

FOR ONLINE USE ONLY





KUSOMA DARASA LA PILI.indd 37 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Baada ya kumtoa bibi mwiba, Jumanne alianza kuondoka. Bibi alimuuliza, unaelekea wapi? Jumanne akajibu, ninakwenda nyumbani. Bibi akamwambia, naomba unisaidie kubeba kuni zangu. Jumanne akajibu, sawa bibi. Jumanne alimsaidia bibi kubeba kuni hadi nyumbani kwake. Bibi alifurahi na kumwambia, wewe ni kijana mzuri.

**Maswali**

**Jibu maswali haya.**

1. Nani aliamka mapema?
2. Bibi alipata tatizo gani alipokuwa porini?
3. Nani alimsaidia bibi kutoa mwiba?
4. Je, Jumanne alikuwa na tabia gani?
5. Hadithi hii inatufundisha nini?
6. Wasimulie wenzako hadithi ya Bibi Chausiku.

**Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali.**

## Kuvuka barabara kwa usalama

Siku moja, shule yetu ilitembelewa na mgeni. Mgeni huyo alikuwa ni **askari** wa usalama barabarani. Alitueleza, kabla ya kuvuka barabara, tunapaswa **kuwa makini**. Tunatakiwa kutazama kulia, kushoto kisha kulia tena. Tukiona hakuna gari lolote ndipo tuvuke. Alitueleza kuwa, tunapotembea barabarani, tutembee upande wa kulia.

FOR ONLINE USE ONLY




KUSOMA DARASA LA PILI.indd 38 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nilimwuliza, kwa nini tunatakiwa kutembea upande wa kulia? Alijibu, kulia, utaweza kuona gari linalokuja mbele yako. Alitueleza, baadhi ya barabara zina **alama za milia**.

Alama hizo ni za mistari myeupe. Alama hizo pia, huitwa alama za pundamilia. Zimewekwa kwa ajili ya watu wanaovuka barabara kwa miguu. Gari linapofika eneo hilo linapaswa kusimama. Mgeni alitueleza kuwa, tukitaka kuvuka barabara tuombe msaada. Msaada wa kuvushwa utolewe na watu wazima. Baada ya kujifunza darasani, mgeni alitupeleka barabarani.



Tulifanya mazoezi ya kutembea upande wa kulia. Aidha, tulielekezwa kuvuka barabara kwa usalama. Wanafunzi wote tulifurahi na kumshukuru mgeni.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Kwa nini tutazame kulia, kushoto tuvukapo barabara?
2. Kwa nini barabara zina alama za milia?
3. Kwa nini mgeni aliwafundisha wanafunzi kuhusu usalama barabarani?

**Andika maana ya maneno ya sehemu A. Chagua jibu sahihi kutoka sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Askari | kuzingatia taratibu za kutembea na kuvuka barabara. |
| 2. Kuwa makini | mtu anayelinda watu na mali zao. |
| 3. Usalama barabarani | ni mistari myeupe inayochorwa kwenye barabara za lami.Mistari hii huwasaidia watu wanaovuka barabara kwa miguu. |
| 4. Alama za milia | hali ya kuwa mwangalifu. |
| | mtu anayefundisha shuleni. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Kusoma kwa ufasaha

**Kusoma herufi, silabi, maneno na sentensi kwa ufasaha**

### Zoezi la 1

Soma herufi hizi kwa haraka na kwa usahihi.

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | y | w | v | u | t | s | r |
| g | h | p | M | z | b | E | f |
| D | a | ch | d | n | w | m | e |
| n | ch | k | u | j | B | G | n |
| i | L | d | b | p | d | o | v |
| w | R | N | L | j | Y | p | y |
| a | ch | H | t | u | e | O | k |
| h | z | h | j | m | A | g | L |
| i | V | t | r | s | d | k | r |
| b | ch | v | P | h | R | j | Ch |
| n | f | M | u | n | u | f | e |
| f | S | a | T | y | g | v | J |
| w | L | O | K | g | l | s | p |
| O | i | t | f | h | r | l | z |
| B | j | ch | F | z | D | o | j |

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 41 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

Soma silabi hizi kwa haraka na kwa usahihi.

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ba | za | du | cha | ga | he | fa | jo | cho | we |
| rwa | le | ha | mbwa | me | fe | la | ma | ju | tu |
| ne | ja | be | pa | dwe | te | ge | chwa | ti | pe |
| lu | che | de | fi | gi | wi | ni | ndwa | hi | po |
| ji | fo | we | nga | bi | no | yo | ka | yu | je |
| ta | mi | le | li | mu | ho | di | lo | mo | na |
| go | lu | pu | chi | so | pi | bo | wu | do | wi |
| hu | wo | ye | lo | mwa | yi | nu | fya | gu | ya |
| pya | za | sa | ze | du | ku | se | zi | bu | ki |
| chu | ke | zu | nza | da | su | ko | si | nywa | wa |

## Zoezi la 3

Soma maneno haya kwa haraka na kwa usahihi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| chafya | duka | mia | miba | kuta |
| goma | zeze | uzi | tui | koo |
| bima | bao | iba | kobe | toka |
| keki | chai | sasa | mwaka | kuti |
| bibi | doa | kosa | mimi | funza |
| cheza | pasi | pweza | baba | saza |
| nyuki | debe | bua | gumu | zizi |

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 42 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| gesi | kutwa | boma | kazi | poa |
| timu | pita | zuka | uza | zako |
| dama | duka | pika | mito | kule |
| nyonga | tamu | meno | buti | mama |
| bima | ota | kama | wahi | ng'ombe |
| moto | taa | dama | kima | jozi |
| dau | muda | wewe | chachu | tai |
| tema | bata | mea | mate | yote |
| kata | yai | bafu | mchwa | chake |
| koka | zamu | chaka | zima | ona |
| saa | pia | kaka | uza | zako |
| lima | choma | tatu | rula | baki |

Endelea kusoma kwa haraka na kwa usahihi

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| bisi | cheka | kaa | chui | piga |
| chanjo | pinda | jema | tiba | kumi |
| bati | kisu | kati | zoa | chako |
| tesa | tuma | dumu | ngozi | jaza |
| lao | gego | soko | bubu | chake |
| kali | zao | chama | zito | nao |
| kasa | kumi | tuta | chura | ota |
| bibi | chema | kali | chuki | pigo |
| tema | kaba | jema | tiba | choma |
| bati | kitu | ua | zima | duma |
| teka | tupa | chaki | goma | jali |
| dai | geti | soma | pigwa | mchwa |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

Soma sentensi hizi kwa haraka na kwa usahihi.

Juma ni mwanafunzi.
Anasoma darasa la pili.
Anasoma Shule ya Msingi Mavuno.
Shule hiyo iko mtaa wa Kichangani.

## Kusoma kwa ufasaha

**Soma habari hii kwa haraka na kwa usahihi.**

### Bustani ya maua

Tunu anasoma darasa la pili. Shule yao ina bustani ya maua. Bustani ina maua meupe, mekundu na kijani. Wanafunzi humwagilia maua kila siku. Tunu amejifunza namna ya kutunza bustani ya maua. Amepanda maua nyumbani kwao. Amemfundisha mama yake kutunza bustani ya maua. Nyumba yao inapendeza.



FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 44 24/07/2021 13:11


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali.**

## Safari ya Mikumi

Zawadi anasoma katika Shule ya Msingi Kidudwe. Anasoma darasa la pili. Wanafunzi walikuwa na safari ya kwenda Mikumi. Walikwenda pamoja na walimu wao. Mikumi ni mbuga ya wanyama. Mbuga hiyo iko mkoa wa Morogoro. Wanafunzi na walimu walikwenda kuona wanyama. Waliwaona wanyama kama tembo, twiga, pundamilia na swala.

Wanafunzi walipokuwa njiani waliimba nyimbo mbalimbali. Zawadi aliwafundisha wenzake wimbo unaohusu mbuga za wanyama. Alianza kutamka maneno ya wimbo kisha sauti yake. Aliimba hivi, Mbuga za wanyama Tanzania. Ya kwanza ni Ruaha, Serengeti, Manyara na Mikumi. Oo! Tanzania oyeeee!



FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 45 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wanafunzi waliimba wimbo kwa furaha, huku wakipiga makofi. Walipofika Mikumi, walipokelewa vizuri. Walipewa mtu wa kuwaongoza. Walitembelea mbuga yote na waliona wanyama mbalimbali. Wanafunzi walipigwa picha kwa ajili ya kumbukumbu.

Baadaye walikula chakula na kunywa vinywaji, kisha wakarudi shuleni. Siku iliyofuata mwalimu alitoa zoezi la kusimulia kuhusu Mikumi. Wanafunzi waliweza kuelezea mambo waliyoyaona katika safari hiyo.

## Maswali

1. Kwa nini wanafunzi walikwenda Mikumi?
2. Wanafunzi walipokuwa njiani walifanya nini?
3. Taja wanyama wanaopatikana katika mbuga ya Mikumi.
4. Kwa nini wanafunzi walipigwa picha walipokuwa mbugani?
5. Wasimulie wenzako kuhusu habari uliyosoma.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 46 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Kusoma hadithi fupi

**Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali.**

### Marafiki watatu

Jalia, Huruma na Mapoe ni marafiki. Wote wanasoma darasa la pili. Jalia ni mtoto mwenye ualbino. Ualbino ni ukosefu wa rangi kamili ya ngozi. Pia ni hali ya macho kukosa rangi kamili. Vilevile ni ukosefu wa rangi kamili ya nywele. Huruma na Mapoe wanampenda sana Jalia. Kila mara wanacheza na kusoma naye. Wanafunzi wengine wanawashangaa kwa kuwa na rafiki albino.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Huruma alisema, Jalia ni binadamu kama sisi. Tunapaswa kumpenda na kumlinda. Hatupaswi kumtenga. Hata walemavu wengine tunapaswa kuwapenda.

Mapoe aliuliza, kwani kuna ulemavu mwingine? Huruma alijibu, ulemavu uko wa aina nyingi. Ulemavu wa akili, viungo, kutokuona na uziwi. Walemavu wanahitaji kupendwa ili waweze kusoma kama sisi. Maelezo ya Huruma yaliwafurahisha wanafunzi. Wakaanza kumpenda Jalia na kushirikiana naye. Walisoma, walicheza na kufanya nae usafi. Jalia alifurahi sana. Aliwapenda wenzake na aliongeza bidii katika masomo. Mwisho wa mwaka wanafunzi walifanya mtihani. Jalia alishika nafasi ya kwanza darasani.

Walimu walimuuliza, kwa nini mwanzoni hukufanya vizuri darasani? Jalia alijibu, wenzangu walikuwa hawataki kusoma na mimi. Sasa wananipenda na kunielekeza vizuri. Ninafurahia sana kusoma na wanafunzi wenzangu. Ninawashukuru sana marafiki zangu Huruma na Mapoe. Wananijali na kunipenda wakati wote.

Jalia alimalizia kwa kusema, walemavu tuna haki. Haki ya kuishi, kupendwa na kupatiwa elimu. Tukipendwa na tukithaminiwa, tunaweza kufanya vizuri.

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 48 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Jalia ana marafiki wangapi?
2. Taja aina za ulemavu zilizoelezwa katika habari hii.
3. Kwa nini mwanzoni Jalia hakuweza kufanya vizuri darasani?
4. Nani alisababisha Jalia kupendwa na wanafunzi wengine?
5. Hadithi hii inatufundisha nini?

## Zoezi la 2

Kamilisha sentensi zifuatazo kutokana na hadithi uliyosoma.

1. Albino ni mtu mwenye ulemavu wa ....................
2. Albino ana haki ya kupendwa,...........na ............
3. Kuna ulemavu wa kutoona,.......,......., na ulemavu wa akili.
4. Walemavu wakipendwa na kuthaminiwa wanaweza ....................

FOR ONLINE USE ONLY



KUSOMA DARASA LA PILI.indd 49 24/07/2021 13:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Soma mazungumzo kisha jibu maswali.**

## Mazungumzo kati ya Tumaini na Adamu

| | |
|---|---|
| **Tumaini** | Adamu, umeonaje somo la leo? |
| **Adamu** | Nimelipenda sana. Mwalimu ametufundisha mambo mazuri. |
| **Tumaini** | Je, unayakumbuka yote? |
| **Adamu** | Mengi ninayakumbuka. |
| **Tumaini** | Unakumbuka nini? |
| **Adamu** | Tumefundishwa kuhusu haki na wajibu wa mtoto. |
| **Tumaini** | Mtoto ana haki gani? |
| **Adamu** | Mwalimu amesema mtoto ana haki ya kuishi. |
| **Tumaini** | Je, haki nyingine za mtoto ni zipi? |
| **Adamu** | Kulindwa, kupata elimu, chakula, malazi na mavazi. |
| **Tumaini** | Je, mtoto ana wajibu gani? |
| **Adamu** | Mtoto ana wajibu wa kuwaheshimu watu wote. |
| **Tumaini** | Je, wajibu mwingine wa mtoto ni upi? |
| **Adamu** | Kuwa na tabia njema na kufanya kazi kwa bidii. |
| **Tumaini** | Asante Adamu, inaonesha unakumbuka mambo mengi tuliyofundishwa. |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

**Jibu maswali haya.**

1. Katika mazungumzo uliyosoma nani alikuwa anauliza maswali?
2. Tumaini na Adamu walifundishwa nini na mwalimu wao?
3. Andika haki za mtoto zilizotajwa katika mazungumzo uliyosoma.
4. Je, mtoto ana wajibu gani?
5. Mazungumzo kati ya Tumaini na Adamu yanahusu nini?

## Zoezi la 3

Kamilisha habari hii kwa kutumia maneno haya.

| | | |
|---|---|---|
| kuishi | ndugu | chakula |
| wazazi | ulemavu | kuwaheshimu |

Mimi ni mtoto. Nina haki ya .......... kama binadamu wengine. Nina haki ya kuwafahamu ........ wangu na .......... zangu. Aidha, nina haki ya kutunzwa. Ninapaswa kupatiwa malazi, .........., mavazi na chanjo. Sitakiwi kubaguliwa kwa sababu ya.......au umri. Mimi kama mtoto nina wajibu wa .......... watu wote.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno uliyopewa.

mavazi binadamu malazi wajibu

1. Nguo zinazovaliwa mwilini huitwa....................
2. .......................... ni mahali pa kulala.
3. Jambo ambalo mtu analazimika kulitekeleza ni .............................

## Zoezi la 5

Andika **NDIYO** kwa sentensi ya kweli. **HAPANA** kwa sentensi isiyo ya kweli.

1. Walemavu wanapaswa kupendwa na watu wote.
2. Watoto hawana haki ya kuishi.
3. Watoto wana wajibu wa kufanya kazi kwa bidii.
4. Wazazi wanapaswa kuwalinda watoto.
5. Watoto wanapaswa kuwaheshimu wakubwa.


FOR ONLINE USE ONLY





KUSOMA DARASA LA PILI.indd 52 24/07/2021 13:11


**Vitabu vingine kutoka**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**


## Darasa la Kwanza



















## Darasa la Pili














## Darasa la Tatu















ISBN 978-9976-61-705-4